Juni 2020

# MIONGOZO NA VIGEZO VYA MWENENDO

## KWA YEYOTE ATAKAYE KUSHIRIKI KATIKA KITENDO CHA KUJIELEZA NDANI YA JIJI LA GRAND RAPIDS

**1. Q. "Kitendo cha Kujieleza" ni nini?**

A. Kitendo cha Kujieleza ni tendo lolote la usemi ama onyesho lilindwalo na Marekebisho ya Kwanza ya Katiba ya Marekani, ikiwa ni pamoja na mkusanyiko wowote ulioratibiwa, wa mtu mmoja au zaidi katika eneo la umma kwa madhumuni ya kushiriki katika yafuatayo, ila si tu:

(1) Vikao na shughuli nyingine za makundi;
(2) Hotuba, maonyesho, maandamano, maadhimisho, mikesha, na matukio mengineyo; ama
(3) Usambazaji wa fasihi, kama vile vipeperushi na vijitabu.

**2. Q. Vipi kuhusu mauzo ya chakula na bidhaa?**

A. Mauzo ya bidhaa, chakula ama huduma nyingine si "Kitendo cha Kujieleza." Shughuli kama hiyo ya biashara si kitendo cha kujieleza kinacholindwa chini ya Katiba, na hivyo kinapaswa kufuata mchakato wa kibali cha Tukio Maalum.

**3. Q. Je, ninahitajika kutoa notisi ya awali kwa Jiji nikiwa na dhumuni la kuratibisha kundi kushirikishi katika Kitendo cha Kujieleza?**

A. Hapana. Hata hivyo, mamlaka ya Jiji inahimiza kila mratibu wa Kitendo cha Kujieleza kutoa taarifa kwa ofisi za Jiji kabla ya kushirikishi kitendo hicho. Notisi itolewayo kwa Jiji husaidia katika utoaji wa maeneo, nguvukazi na rasilimali nyinginezo.

**4. Q. Je, ninahitajika kupata Kibali cha Tukio Maalum ili kushiriki katika Kitendo cha Kujieleza?**

A. Hapana. Hata hivyo, washiriki wote wanahitajika kufuata sheria zote, kanuni na Vigezo vya Mwenendo vilivyojumuishwa katika Muongozo huu.

**5. Q. Je, ninaweza kuandamana mtaani ama kwenye njia kuu bila kuwa na kibali?**

*A.* Hapana, vibali husika vitahitajika. Mtu yeyote yule anayezuia ama kuvuruga shughuli za barabara katika maeneo ya umma anavunja sheria: "*Mtu, asiye na mamlaka, hatapaswa kuzuia, kuvuruga, kukwamisha, ama kuingilia mkondo*

*wa kawaida wa magari au watembea kwa miguu katika mitaa ya umma ama njia kuu zilizopo ndani ya jimbo hili, kwa kutumia vizuio, kitu, au kifaa, ama kwa kutumia mtu wake."*

MCL 257.676b. Jiji linakuhimiza kupanga washiriki wote pembezoni mwa barabara na kufuata kanuni pamoja na udhibiti wa barabarani.

**6. Q. Vipi kama ninataka kuendesha gwaride, ama vinginevyo kuwepo mtaani?**

A. Unapaswa kuwasiliana na Ofisi ya Matukio Maalum kupata kibali.

**7. Q. Je, iweje kama ninataka kuratibu maandamano mtaani kufuatia tukio la hivi karibuni, na sina muda wa kutosha kupata Kibali cha Tukio Maalum?**

A. Kama tukio hilo litafanyika mtaani, basi kibali kitahitajika. Kufungwa kwa mitaa huhitaji mikakati. Kingo na wafanyakazi wa Jiji hawana budi kuwepo. Maofisa wa polisi huhitajika kuhakikisha usalama kwa raia, hasa katika makutano ya njia. Huduma zote hizi huhusisha gharama. Mtu yeyote yule anayetaka kutumia njia za Jiji anapaswa kuwasiliana na Kitengo cha Jiji cha Matukio Maalum katika masaa ya kazi, ama GRPD nje ya masaa ya kawaida ya kazi. Vinginevyo, kama kundi linahitaji kufanya maandamano bila kuwa na kibali, washiriki wake watabidi kubaki pembezoni mwa njia na kuheshimu vifaa vyote vya udhibiti barabarani.

**8. Q. Ada zilizopo ni zipi?**

A. Hakuna ada zozote katika Vitendo vya Kujieleza. Kama utahitaji kuwa na Kibali cha Tukio Maalum kwa ajili ya mkusanyiko wako, tafadhali wasiliana na Ofisi ya Matukio Maalum.

**9. Q. Sasa kwanini nihitaji Kibali cha Tukio Maalum, kama si lazima kuwa nacho?**

A. Kama unahitaji kuhifadhiwa eneo fulani kwa ajili ya kundi lako, inapendekezwa kuwa na Kibali cha Tukio Maalum. Kwa mfano, kama unataka kutumia jukwaa lililopo Rosa Parks Circle kufanya kitendo cha kujieleza bila kuwa na kibali, basi utapaswa kuelewa kuwa jukwaa hilo litaweza kutumika na WOTE ambao huenda wangetaka kuzungumza. Endapo kama ungependa Jiji lifunge njia, ama ungehitaji kupangisha kifaa kutoka kwa Jiji, ama kuhitaji wafanyakazi wa Jiji kufanya kazi nje ya muda wao wa kazi, basi huduma hizo zitabidi kuratibiwa kupitia mchakato wa Kibali cha Tukio Maalum.

**10. Q. Je, ninahitaji kukata bima?**

A. Hapana. Lakini iwapo kama utaamua kupata Kibali cha Tukio Maalum, basi bima inaweza ikahitajika kama tu vile inavyohitajika kwenye Matukio mengine Maalum.

**11. Q. Je, vipi kama nikaratibu Kitendo cha Kujieleza na ikawa mtu mwingine amekwisha hifadhi eneo hilo hilo kwa ajili ya Tukio Maalum?**

A. Huu ni mfano mzuri wa kwanini notisi ya awali kwenda kwa Jiji ni muhimu kwa kila mtu. Kama eneo husika limeshawahiwa na wengi ama halifai (yaani, kuna ujenzi unaoendelea, ama uwezo wa eneo hilo kubeba kiasi cha watu si toshelevu kufaa umati unaotarajiwa), basi wafanyakazi wa Jiji wanaweza kuwasaidia waratibu kupanga mipango mbadala inayofaa kutatua changamoto hizo.

Zingatia kwamba utoaji wa notisi kwa Jiji kuhusiana na tukio lijalo si uwekaji wa hifadhi. Ni Kibali cha Tukio Maalum pekee ndicho kitakachoweza kuhifadhi eneo kwa ajili ya kundi lako.

**12. Q. Je, vipi kama nikaratibu Kitendo cha Kujieleza na kundi tofauti likafika katika eneo hilo hilo likiwa na mitazamo tofauti? Je, polisi watanyamazisha onyesho hilo pingamishi? Je, kundi hilo jingine linaweza likazima tukio langu?**

A. Hapana na hapana. Sheria inawaruhusu watu wenye malengo na mitazamo tofauti kukusanyika kwa amani na kuelezea mitazamo yao. Kundi shindanishi zinapotokea katika eneo moja wakati mmoja, Jiji linaruhusiwa na sheria kugawa eneo hilo kwa usawa, sawasawa na idadi ya malengo yanayoadhirishwa. Hili linamaanisha kwamba, ikiwa kama kuna makundi mawili yenye mitazamo tofauti, Jiji linaweza kugawa eneo hilo katika sehemu mbili. Kama kuna makundi matatu tofauti, eneo litagawanywa katika sehemu tatu, vivyo hivyo. Kwa mara nyingine, tunahimiza waratibu wote wa matukio kutoa taarifa kwa Jiji kuhusiana na mipango iliyopangwa na kukata kibali cha Tukio Maalum kuhifadhi eneo la kutosha kwa ajili ya makundi yao.

**13. Q. Nimesikia kwamba kundi lingine linaweza likajitokeza na kwamba litaleta uhasama kwa kundi langu. Nifanye nini?**

A. Tafadhali lijulishe Jiji kama una taarifa ya aina hii. Wasiliana na Kitengo cha Polisi katika hali zisizo za dharura, ama piga 911 kwenye hali za dharura. Jiji litafanya kazi kuhakikisha uwepo wa tukio salama na linalofuata sheria kwa wote watakaohusika.

**14. Q. Nina Kibali cha Tukio Maalum. Je, jiji litamuondoa mtu yeyote atakayejitokeza kujaribu kuvuruga tukio langu?**

A. Kama tukio lako halina kiingilio na li wazi kwa watu wote, Marekebisho ya Kwanza yatalinda kitendo cha kujieleza. Hata hivyo, endapo kama kitendo hicho kitakiuka Vigezo vya Mwenendo kiasi cha mtu kuvuruga tukio husika, basi utapaswa kuwasiliana na polisi. Polisi hawatamuondoa mtu kutoka kwenye tukio lako kwa sababu tu wewe ama mmoja wa washiriki wako hawapendi ujumbe unaoelezwa na mtu huyo.

**15. Q. Nina Kibali cha Tukio Maalum. Tukio hili halina kiingilio na ni wazi kwa watu wote. Kuna mtu anataka kuweka mkusanyiko wake ndani ya mipaka ya eneo la tukio langu. Nifanye nini?**

A. Kama mratibu wa tukio hilo hataki kusanyiko hilo lifanyike ndani ya mipaka ya tukio lake, basi wanaweza kutakiwa kuondoka. Mtu huyo anaweza kuruhusiwa kuweka kusanyiko lake nje ya mipaka ya tukio hilo, almradi tu asiingiliane na umati wa watembea kwa miguu.

**16. Q. Nina Kibali cha Tukio Maalum. Je, mtu yeyote anaruhusiwa kugawa vipeperushi ama vijitabu ndani ya tukio langu maalum?**

A. Ndio. Kama tukio lako halina kiingilio na li wazi kwa watu wote, basi jambo hili litalindwa na hotuba ya Marekebisho ya Kwanza.

**17. Q. Nina Kibali cha Tukio Maalum. Je, vipi kama mtu ataibuka kwenye tukio langu akiwa ameshikilia mabango?**

A. Kama tukio lako halina kiingilio na li wazi kwa watu wote, jambo hili litalindwa na hotuba ya Marekebisho ya Kwanza.

**18. Q. Je, Tukio langu la Kujieleza linaweza kujumuisha vifaa ama zana za kupaza sauti?**

A. Vifaa vya kupaza sauti vinaweza kutumika ndani ya jengo la umma almradi tu sauti isizidi “wastani wa kiwango cha mazungumzo” umbali wa futi 100 kutoka kwenye chanzo cha sauti. Vifaa vya muziki pia vinaruhusiwa. Hata hivyo, Agizo la Kelele la Jiji lina matakwa ya “masaa ya ukimya” kati ya saa 10:00 jioni na 7:00 asubuhi. Tafadhali zingatia makazi na biashara zinazozunguka eneo lako na muda wa siku utakao tumia vifaa vya kupaza sauti. Ofisi ya Matukio Maalum inaweza pia kutoa vibali vinavyoruhusu utumizi wa kifaa cha sauti na viwango vya juu zaidi vya sauti.

Yaliyopo hapa ni baadhi ya maelezo muhimu kuhusiana na agizo la kelele unayopaswa kuzingatia unapoweka mipango ya Kitendo chako cha Kujieleza:

Kifungu.9.63 Kelele

Iliyokatazwa

Hakuna mtu anayeruhusiwa:

* * *

(2) Kati ya saa 10:00 jioni na saa 7:00 asubuhi, kufungulia ama kuwasha redio yoyote, runinga, kifaa cha kieletroniki cha sauti, ngoma, kifaa cha muziki, ama kifaa kinachopaza sauti kiasi cha sauti hiyo kusikika kwenye mipaka ya eneo lililohifadhiwa kwa ajili ya makazi.

* * *

(4) Kuwasha kifaa chochote kinachokuza sauti katika jengo la umma ama maeneo ya umma, inayozidi wastani wa kiwango cha mazungumzo katika umbali wa futi mia moja (100) au zaidi, kwa wima au kwa usawa, kutoka kwenye chanzo husika.

* * *

(9) Kati ya saa 10:00 jioni na saa 7:00 jioni, kupayuka, kupiga yowe, kuita, kupiga kelele, kupiga mluzi, ama kuimba kwenye njia za hadhara, ama karibu na njia za hadhara, kwa sauti ya juu kiasi cha kusikika na watumiao njia hiyo.

Unaweza kutazama mengineyo ya agizo hili hapa.

# VIGEZO VYA MWENENDO

Watu wote wanaoshiriki katika Kitendo cha Kujieleza, bila kujali kama Kibali cha Tukio Maalum kimekatwa au la, watapaswa kufuata vizuizi vya muda, eneo na vya muundo kama ifuatavyo:

1. Washiriki hawatapaswa kuzuia ufikivu wa majengo, wala kuvuruga uingiaji na utokaji wa kwenye maegesho ya magari, hifadhi, kituo ama tukio lolote. [Sheria za Jiji Kifungu. 9.132, MVC 257.676b.] Kamwe hakuna mshiriki yeyote atakayeruhusiwa kuvuruga uingizi na utokaji wa magari au watu kwenye maeneo ya hospitalini, vituo vya uzimaji moto, ama kituo kingine cha ushughulikiaji dharura.

2. Washiriki hawataruhusiwa kuzuia magari ama watembea kwa miguu. [Sheria za Jiji Kifungu. 9.132, MVC 257.676b.] Katika hali yoyote, hakuna mshiriki yeyote atakayeruhusiwa kuvuruga ufikivu wa makutano yoyote ya njia, ikiwa ni pamoja na miteremko ya njia, barabara na madaraja yanayoendea njia kuu hizo.

3. Kitendo cha Kujieleza hakitapaswa kujumuisha shughuli yoyote inayovunja sheria. Washiriki wanapaswa kufuata sheria, amri, maagizo, kanuni zote za Serikali, Jimbo na za Mitaa.

4. Mtu yoyote anaweza kutumia vifaa vya kupaza sauti katika jengo la umma almradi tu sauti hiyo isizidi wastani wa kiwango cha mazungumzo katika umbali wa futi 100

au zaidi, kwa wima au kwa usawa, kutoka kwenye chanzo, kulingana na agizo la kelele la Jiji ama kama ilivyoidhinishwa kwenye Kibali cha Matukio Maalum. [Sheria za Jiji Kifungu. 9.63(-4) (Kelele) ama 4.207 (Matukio Maalum)]

5. Kitendo cha Kujieleza hakitapaswa kujumuisha utupaji taka, ama ubandikaji karatasi kwenye jengo la Jiji, miundombinu ama katika vijia vya kando ya barabara. Washiriki watapaswa kuwajibika kuokota chapisho zozote zilizodondoshwa kwenye ardhi izungukayo maeneo ya usambazaji. [Sheria za Jiji Kifungu. 9.26.]

6. Maegesho ya magari, njia za barabara na gereji hazifai kutumika kuwa maeneo ya Kitendo cha Kujieleza, na uwekaji wa vipeperushi kwenye vioo vya magari hautaruhusiwa. [Sheria za Jiji Kifungu. 9.26.]

7. Kitendo cha Kujieleza sharti kifanyike ndani ya masaa ya kawaida ya kazi ya jengo husika litakalotumika. [Sheria za Jiji Kifungu. 3.8 (Hifadhi)]